

Ukweli Hauna Kutu

Pambazuko

Toleo Namba 015

Jumatatu Oktoba 17-23, 2022

Uk.2 - Siasa kamwe isiandae mawakili



**TanESCO
yakoleza
umasikini
Uk.13**

**Walilia
fedha
zao
Ikulu**

Uk.6 - Tumdai Samia viatu vya Nyerere

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Siasa haifai kuandaa mawakili

ZAIDI ya wiki moja sasa, Tanzania imegubikwa na mjadala mkubwa kuhusu ufaulu hafifu wa wanafunzi wa Shule Maalum ya Sheria kwa Vitendo ya Tanzania (Law School).

Sehemu kubwa ya mjadala huo kupitia mitandao ya kijamii, makomangano na mikutano isiyokuwa rasmi, inachukua sura mbili; moja ikilaulu wanafunzi kwa kushindwa “kukaza buti” kufaulu mitihani, nyingine ikieleza madai ya walimu “kuwakazia” wanafunzi kwa kutunga mitihani migumu.

Zote hizi mbili ni sababu ambazo zinatawala, huku ikionekana kwamba wengi wanakubaliana na wale wa upande wa wanafunzi kushindwa kuweka bidii katika elimu ya vitendo inayofunzwa shuleni hapo.

Kwamba wanafunzi wameshindwa kufahamu lengo hasa la kuwepo shuleni hapo, wakiamini mambo ni kama kule walikotoka - vyuoni ambako ufaulu unaweza kumwangukia yoyote, hata yule asiyekuwa na bidii darasani, ilimuradi anajua “njia” za kufaulu mbali na kujisomea.

Siyo jambo la siri na wala siyo habari tena, kwamba vyo vingi vya elimu ya juu, vimekuwa “vikizalisha” wanafunzi wasiokuwa na uwezo wa kushindana katika soko la ajira kwa kuwa walimu wengi na idadi kubwa ya wanafunzi wote wamegubikwa na “janjajanja” ya kushinda mitihani badala ya kujaza na kujazwa maarifa.

Sasa hawa, kwa kuwa ni kundi kubwa, wanapoingia shule maalum ya sheria kwa vitendo, wanakosa mwanya

wa ujanjaujanja na hapo ndipo wanaona shule ngumu na mwisho kwenye mitihani wanashindwa.

Lakini wale wanaoweka bidii ya kusoma, ndiyo hao tunawaona wakifaulu na kuja kuwa mawakili, mahakimu na majaji wenye kutukuka na siyo wale janjajanja, ambao huiacha taaluma ya sheria uchi kwa kutojua hata sheria waliyoisomea.

Inasikitisha sana kuwepo kwa malalamiko ya mahakimu kwamba baadhi ya wanafunzi wa sheria kutoka vyoju vikuu wanaofika mahakamani kujifunza, wanashindwa hata kuandika kiapo (affidavit) wakati wamekaa chuoni kwa miaka mitatu. Ni aibu.

Malalamiko ya mahakimu siyo ya jana wala juzi, yamekuwepo kwa muda, hata kama hawasemi kwenye vyombo vya habari, lakini yapo na yanafikishwa hata vyuoni huko, lakini ni kama hayafanyiwi kazi. Mazao mengi yanakuwa bado hovy!

Kinachosikitisha zaidi, katika mjadala hiyo ya kadhia ya ufaulu hafifu, wanaonekana wanasiasa wakishabikia na kulaani kwamba “huenda wanafunzi wanaonewa.”

Sisi katika Pambazuko tunasimama hadharani na kueleza kwamba dhana hii ya wanafunzi kuonewa inayobebwa na baadhi ya wanasiasa, ni mfu. Ni njia ya kuendelea kulea uzo ambao wanasiasa haohao wameukumbatia na kulifikisha taifa letu hapa lilipo; kwenye mkwamo mkubwa katika maeneo mengi ya utendaji.

Hebu wanasiasa waache wanataaluma wanaoandaliwa kulumikia taifa, waive haswa kabla ya kuja kuwa mawakili, mahakimu na majaji wetu ili watetee na kuhukumu kwa haki.



Jisajili kupata Pambazuko bure

Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno “**HABARI**” kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

Pia unaweza kujisajili kwa kutumia Email hii: pambazuko1@protonmail.com ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno “**HABARI**” na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



“Mafanikio hayaji kama ajali, bali huja kwa kazi ngumu, uvumilivu, kujituma, kujifunza, kujitoa na zaidi ya yote upendo kwa kile unachofanya au kujifunza kufanya” –

Msemo maarufu kwa kabila la Wasukuma.

Ujinga wetu mtaji wa matapeli

Na Dkt. Bullet RUHINDA

KATIKA juma lילוisha jana, kumekuwepo na taarifa mbalimbali za madai ya watu kutapeliwa mamilioni ya pesa na kampuni ya mtandaoni iitwayo Kalynda.

Inasikitisha sana kuona watu wanapoteza pesa zao walizozitolea jasho jingi, lakini kusikitika hakumzuii mtu kujiuliza na kushangaa watu hawa kwa nini wametapeliwa?

Wahanga wa utapeli huo ni watu kutoka kada mbalimbali; waajiriwa na wasioajiriwa. Ajabu zaidi ni kwamba kuna hata maprofesa waliotapeliwa.

Kabla ya kuangalia tumeanguka wapi, ni vyema tujitafakari wapi tumejikwaa. Katika dunia huria tuliyo, kila kitu ni fursa. Kutojua au kukosa kwetu taarifa sahihi, ni fursa kwa wengine.

Kalynda wametumia fursa ya ujinga wetu kututapeli, tena wamewatumia wenzetu na vyombo vya habari kutuaminisha kwamba wanatoa faida kubwa, kumbe wametutegeshea ndoano.

Vijana wenge kwa sasa na hata watu wazima wamepatwa na ugonjwa wa kucheza kamari (maarufu betting). Kudhani kwamba bahati nasibu (soma kamari) inaweza kukutajirisha. Yaani kuandika Arsenal itashinda mabao mawili dhidi ya Manchester City - initajirisha kuliko mtu anayefanya kazi saa 12 kwa siku.

Tunashindwa kujua wanaoshinda bahati nasibu hiyo ni moja kati ya watu maelfu, na wao ndio wanatumika kama chambo kutunasa.

Watanania wengi tunapenda kupata utajiri bila kufanya kazi. Kwamba kesho baada ya kushinda betting, basi nitakuwa na nyumba, magari na mashamba! Ajabu.

Mwandishi nguli wa Marekani Sidney Sheldon, katika kitabu chake maarufu "If Tomorrow Comes," anasema mtu hawezi kutapeliwa kama siyo mzembe na hana tamaa ya utajiri wa haraka!



Pesa za mfano

Watanania wengi hayo ndio matatizo yetu. Tamaa inatufanya wajinga! Wengi wetu tunafanya kile kinachofanywa na baadhi ya wanyama kujipeleka machinjioni. Ni sawa na Mbwa hujipeleka kwa chatu kumezwa badala ya kukimbia!

Tunashindwa kujiuliza, huyu Kaylinda anapata faida gani kwa kunitajirisha mimi? Yaani mimi nichukue bidhaa kwake kisha anilipe!

Nashangaa hata maprofesa ambao kazi yao ni kutuelimisha, wameingia mkenge huo! Kama huo ndio mwendo wetu, yaani hata profesa anatamani kupata vya bure bila jasho, je tunatengeneza kizazi gani?

Kwa kizazi hiki cha betting tulichomo - miaka kumi ijayo tutakuwa wapi? Je, elimu tuliyoonyo inatupatia maarifa ya kukabiliana na utapeli kama huu au ndio kila siku kuilaumu serikali kwamba ilitoa vibali kwa kampuni za kitapeli!

Kwa nini kabla ya kutapeliwa hatuendi kutoa taarifa bali tunaibuka baada ya kupigwa? Tujitafakari vya bure vinaua, vitabu vitakatifu vinasema "Na asiyefanya kazi asile."

Kaylinda iwe ya mwisho "kutupiga," la sivyo, tukikubali kupigwa - tusilie.

Uwakili siyo ‘mchezomchezo’

Na Dunstan MTAGAHYWA

KUMEKUWEPO na mjadala kunoendelea nchini Tanzania kuhusu idadi ndogo ya wanafunzi wa Shule ya Sheria wanaofanikiwa kupata hadhi ya uwakili.

Msingi wa mjadala huo ni kushindwa kwa wanafunzi kupata uthibitisho wa kuwa mawakili baada ya kufanya mitihani ya shule hiyo iliyoko Dar es Salaam.

Matokeo yanayolalamikiwa ni yale ya mwaka huu ambapo wanafunzi jumla ya wanafunzi 651 katika mitihani hiyo; 26 wamefaulu, 342 wametakiwa kurudia baadhi ya masomo, huku wengine 265 wakielezwa “kufeli.”

Kutokana na malalamiko ya wanafunzi na wadau, serikali iliamua kuunda tume maalum itakayoongozwa na Dkt. Harrison Mwakymbe, mwanasheria nguli. Imepewa siku 30 kukamilisha kazi hiyo na kuwasilisha serikalini.

Bila kutetea upande wowote; shule na wanafunzi - nieleze kuwa masomo katika shule hiyo ni magumu na kushinda mitihani yake, lazima mwanafunzi kwanza “ajikane.”

Ni lazima mwanafunzi aache “kuchezacheza,” aweke muda wake mwingi kujisomea, kuwa karibu na walimu kwa maana ya kuuliza pale anapokwama kuelewa, apate rejea ya vitabu, maandiko na makala nyingi kuhusu namna sheria kwa vitendo inavyopaswa kuwa. Kinyume na hapo, kushindwa ni kitu rahisi sana.

Ninachoamini ni kwamba mwanafunzi akifanya hayo na kuweka bidii kubwa darasani na kushirikisha mawakili wasomi katika changamoto za elimu hiyo, huku akiacha kujihusisha na mambo mengine, hakika atashinda mitihani hiyo na hatimaye kuwa wakili.

Sioni kama kuna kuonewa kwa wanafunzi kama ambavyo inaweza kuonekana kwa wanafunzi wenyewe na hata jamii.

Ileweke kuwa kila mtu anavuna



Dkt. Harrison Mwakymbe

anachopanda. Mbona baadae wanaosemekana kushindwa wakirudia mitihani wanashinda? Tangu shule hiyo ianze kuna ongezeko la zaidi ya mawakili elfu kumi, je, hao walisomea shule ipi?

Ukweli ni kwamba masomo yanayofundishwa pale shuleni ni mkusanyiko (na ziada kidogo) wa mambo mengi yaliyofunzwa vyuoni kwa njia ya nadharia, na sasa kufunzwa kwa vitendo – kwa muda wa miezi mitano tu. Hivyo, ni kazi ya kujifunga mkanda na kuelewa. Kamwe siyo kukariri.

Wengi wanashindwa wanapoingia katika shule hiyo kwa kudhani kwamba mambo ni mepesi na kupata muda wa kuchezacheza, inapokuja mitihani wanashindwa kufaulu kama vile hawajawahi kusomea sheria huko walikotoka.

Ndiyo maana, wale wanaoshindwa mara ya kwanza, wakirudia mitihani - na kuongeza bidii, hushinda kwa kuwa wanang’amua kwamba katika shule hiyo, hakuna “mchekeke mkwe.”

Ikiwa matokeo ya Tume ya Dkt. Mwakymbe yatawekwa hadharani, wahusika wakuu, kwa maana ya wanafunzi wanaweza kuficha nyuso zao kwa “madudu” yatakayobainika kuyaandika katika mitihani yao.

Mwandishi wa makala haya yaliyohaririwa kukidhi hadhi ya Pambazuko, ni wakili wa Mahakama Kuu Tanzania.

Tum dai Samia viatu vya Nyerere

Askofu Dkt. Benson Bagonza

Ni miaka 23 tangu Baba wa Taifa letu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere afariki dunia.

Kwa urefu wa maisha yake na muda alioliongoza Taifa letu, Mwalimu aliweka msingi na viwango vya uongozi. Ni sahihi bila hofu yoyote nikisema, viwango vyake alivyoweka katika nyanja za uongozi, uzalendo, uadilifu, maono, umajumui, diplomasia na siasa, ndicho kiatu tunachohitaji daima kujipima kama tunaenea.

Naelewa kuwa Mungu huumba mtu mmoja pekee na ndiyo maana tunachukuliwa alama za vidole kwa sababu kila mtu anafanana peke yake.

Kwa hiyo, siyo haki kum dai mtu afanane na mwingine wala siyo sawa mtu kuteseka akihangaika kufanana wala kulingana na mwingine.

Ni haki na sahihi mtu kuridhika na jinsi Mungu alivyokuumba na vipawa alivyompa. Tusidaiane ambavyo hatukupewa wala tusijipe deni tusiloweza kulipa.

Mwalimu Nyerere alikuwa na upekee tusioweza kuudai kwa yeyote. Tunaweza kudai viwango vya uongozi wake pasipo kuwalazimisha viongozi wetu wafanane naye.

Aidha, tunaweza kumfanya Mwalimu Nyerere kuwa kipimo na kiwango cha kutathmini utendaji wa viongozi wetu wa sasa kwa sababu tu, Mwalimu ni muasisi wa taifa letu aliyeweka misingi tuliyokulia tukiwa taifa moja.

Ni kwa ajili hiyo, naamini siyo sahihi kwa viongozi waliomfuata Mwalimu kuanza kupimana vifua na kugeuzana mifano ya kuigana.

Mfano pekee tulio nao ni Mwalimu na ingefaa viongozi wajipime katika viatu vyake.

Nayasema haya kwa sababu kadhaa; umoja wa taifa letu umeyumba baada ya Mwalimu kuondoka. Waliouyumbisha hawawezi kuigana.

Pia heshima yetu mbele ya mataifa



Rais Samia Suluhu Hassan

imeshuka baada ya Mwalimu kuondoka. Walioishusha wasiigane.

Halafu maendeleo ya vitu yako juu ya maendeleo ya watu. Waliofanya mabadiliko haya hawapaswi kuigana.

Zaidi sana, Mwalimu alipigania uhuru wa taifa na watu wake. Hivi sasa uhuru wa watu haulindwi, bali uhuru wa viongozi.

Kama haitoshi, chini ya Mwalimu, cheo kilikuwa ni dhamana na utumishi kwa umma. Siku hizi cheo ni ajira, utumishi kwa mteuzi na fadhila kwa mteuliwa.

Wakati wa Mwalimu wapigakura waliamua nani aongoze. Hivi sasa wahesabu kura na watangazaji ndio wanaoamua nani awe kiongozi.

Chini ya Mwalimu, vyombo vya dola vililinda raia na mali zao. Hivi sasa vinalinda viongozi na vyama vya siasa. Vyombo vya ulinzi vina sauti kuliko umma hata kama vinaitwa vyombo vya wananchi.

Mabadiliko haya yanatudai kitu kimoja; viatu vya Mwalimu ndicho kipimo na kiwango cha uongozi.

Ileweke kuwa viatu vya Mzee Ali Hassan Mwinyi, Benjamin Mkapa, Jakaya Mrisho Kikwete na John Pombe Magufuli tusim dai Rais Samia Suluhu Hassan, huyu tum dai viatu vya Mwalimu Nyerere.

Uishi milele mioyoni mwetu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Baba wa Taifa la Tanzania.

Makala haya yaliandikwa mwaka jana, lakini kwa uzito, tunatumia tena mwaka huu na tutaendelea kuwa nayo kila mara.

Wawekezaji watamani Zanzibar

Na Mwandishi WETU

ENDAPO jitihada za sasa zinazofanywa na Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi, za kukuza uchumi, nchi hiyo inaweza kuwa kituo kikuu cha kusambaza huduma za nguvu ya teknolojia na mawasiliano katika ukanda wa Afrika.

Haya yamebainika hivi karibuni baada ya kampuni kadhaa za teknolojia kuonyesha nia ya kuwekeza katika visiwa hivyo, baada ya kuwepo kwa mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji.

Tayari Rais Mwinyi ameweka bayana kwamba wawekezaji wenye uhitaji wa ardhi na huduma zingine, kutokwamishwa kwa visingizio vyovyote, huku akiwataka watendaji wa serikali anayoongoza kurahisisha zaidi kupatikana kwa vibali.

Hivi karibuni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifikia makubaliano na kampuni kubwa na maarufu ya Wasoko, ambayo ni kinara kuendesha biashara ya kuunganisha – kwa njia ya mtandao, wateja na wazalishaji wa bidhaa bila kujali mipaka wala umbali.

Inaelezwa kuwa Wasoko imeamua kuwekeza Zanzibar baada ya kubaini ujio wa kampuni kadhaa zenye lengo la kuwekeza mifumo muhimu ya kurahisisha biashara kwa njia ya mtandao.

Waziri wa Nchi, Uchumi na Uwekezaji wa Zanzibar, Mudrick Soraga ameliambia Pambazuko kwamba Zanzibar kwa sasa “inakimbizana” kuhakikisha uchumi wake unakua kwa kasi, watu wanapata ajira na vijana wanapata elimu ya kujifunza zaidi kutoka kwenye kampuni za kimataifa.



Mhe. Mudrick Soraga

Anasema milango ya kuwekeza Zanzibar imefunguliwa na yeyote, anayefanya biashara halali na zenyewe kukuza uchumi wetu anakaribishwa kuwekeza mtaji wake bila kubhughdhiwa na mtu wala taasisi yoyote.

“Tunafuraha kushirikiana rasmi na Wasoko na makampuni mengine ya teknolojia yanayokuja Zanzibar ili kuunda sera na mipango ambayo itaibadilisha Zanzibar kuwa kituo kikuu cha teknolojia kwa Bara la Afrika,” alisema

Soraga wakati akiikaribisha Kampuni ya Wasoko.

Soraga alisema serikali itaboresha utoaji wa viza za kazi kwa wafanyakazi wenye ujuzi wa teknolojia na kutoa mazingira mazuri na kuwezesha kwa kampuni zozote, zikiwamo za teknolojia kufanya kazi katika nchi hiyo yenye utalii maarufu duniani.

Tangu kuingia madarakani, Rais Mwinyi amekuwa akikutana na wawekezaji wakubwa akiwa Zanzibar au akisafiri kuwafuata huko ughaibuni kwa lengo la kuwaalika kwenda kuwekeza Zanzibar bila kuhofia “kuvurugwa” kwa uwekezaji wao.

Kampuni ya Wasoko inatajwa kuwa na rasilimali zinazofikia dola za Maeraki milioni 652 hadi kufikia Mei mwaka huu na kwamba mtaji wake unakua kwa kasi.

Nguvu za kugawa madaraka

Na Askofu Dkt. Stephen MUNGA

KATIKA sehemu hii tutaendelea kutazama ni nani mwenye madaraka ya juu na hivyo aweze kuyagawa ili kujenga miundo na mifumo ya utawala wa taifa.

Aina ya utawala uliopo ndiyo huamua ni nani ana nguvu. Ikiwa utawala uliopo ni wa kifalme, basi mfalme ndiye mwenye nguvu.

Ikiwa ni utawala kidini/kimungu, basi kuhani mkuu na wateule wa dini hiyo ndio wenye nguvu. Ikiwa utawala ni wa kiimla, basi aliyejinyakulia madaraka ndiye mwenye nguvu. Aina hizi zote hulindwa kwa katiba na sheria na nguvu zote za dola hutumiwa kulinda tawala hizo na matakwa yake.

Hapa napenda kujishughulisha na ugawaji wa madaraka katika aina ya utawala wa kidemokrasia ambao mataifa mengi siku hizi hupenda kujiita hivyo.

Ni vyema ieleweke kuwa katika familia ya utawala wa demokrasia, zipo aina kadhaa tofauti ambazo hukubaliana juu ya hoja ya msingi juu sifa kuu ya demokrasia.


Hoja hiyo ya msingi ni kwamba demokrasia ni utawala wa watu kwa ajili ya watu.

Aina za demokrasia zilizopo mezani ni demokrasia ya moja kwa moja, demokrasia ya uwakilishi, demokrasia ya kikatiba, na siku hizi inatokeza demokrasia ya ufuatiliaji (monitory democracy).

Sisi Tanzania tunafuata aina ile ya demokrasia ya uwakilishi. Hii maana yake ni kwamba watu wanachagua wawakilishi wao ambao wanapewa dhamana ya kuona kwamba taifa linatawaliwa ipasavyo.

Hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba wawakilishi hao wanatunga sheria na miongozo ya kuhakikisha kwamba nchi inatawaliwa kwa mujibu wa katiba na sheria zinazofanua matakwa ya katiba ya nchi.

Katiba yenyewe katika mtazamo huu huonekana kama sheria ya juu



Katiba

inayolinda mkataba wa utawala kati ya watu na watawala. Kwa hiyo katiba ni maagizo ya watu yanayoelekeza jinsi taifa litakavyotawaliwa; na humo kuna maelekezo yote juu ya miundo na mwongozo wa ujenzi wa mifumo kama inavyowapendeza wenye taifa.

Ili kulinda haki na kuhakikisha uwiano wa madaraka kwa njia ya mgawanyo wa madaraka, wananchi wametengeneza mihimili mitatu; utawala, uwakilishi na mahakama. Kwa njia moja au nyingine mihimili hii yote mitatu inatakiwa iwekwe na watu. Iko hivyo ili kuzuia mhimili mmoja kupoka madaraka ya mingine.

Katika muundo huo inawezekana mhimili mmoja ukawa dhaifu katika kipindi fulani, lakini bado nguvu ya mihimili miwili iliyobaki ikavusha taifa katika nyakati ngumu. Hatari kubwa ni pale inapotokea ama mihimi miwili au yote kuwa dhaifu.

Hapo ndipo ambapo nguvu ya wenye nchi lazima iingie kufanya mabadiliko ya haraka. Kwa maelezo hayo inaonekana wazi kwamba katika utawala wa kidemokrasia, nguvu imo mikononi mwa wananchi.



Akili mpya itumike kukabili utapeli

MIONGONI mwa kauli ninazozirudia mara kwa mara kwenye mitandao ya kijamii ni hii, najinukuu - “kwa akili hizi (miongoni mwa Watanzania wengi), hata katiba mpya ikipatikana kila baada ya saa 24 itakuwa kazi bure. Kinachohitajika zaidi ni akili mpya.”

Na kauli hii huwakera sana wanaharakati wanaopigania katiba mpya. Hata hivyo, kauli hiyo haimaanishi kuwa katiba mpya siyo muhimu au haihitajiki, bali ni angalizo tu kwamba, “katiba mpya katiba akili hizihizi” inaweza kusababisha isiwe na ufanisi.

Kilichonifanya nikumbuke kauli hiyo ni tukio linalotawala anga za habari nchini Tanzania kuhusu kampuni moja iliyokusanya mamilioni (au ni mabilioni?) ya shilingi za watu mbalimbali, kwa ahadi za “kupanda mbegu” kisha utajiri huo waja kama mvua ya ghafla.

Tukio hilo likanikumbusha mlongo mrefu wa matukio mengine huko nyuma ambapo maelfu kama siyo mamilioni ya Watanzania walitapeliwa fedha zao kwa tamaa ya kupata fedha za “chapchap.”

Ukifuatilia wengi wa wanaolalamika kwa wametapeliwa na kampuni hiyo, ni wahanga wa utapeli wa kampuni nyingine ambazo zilikuja na ahadi hizohizo za utajiri wa haraka haraka.

Japo wenye kampuni husika hawawezi kukwepa lawama kwa utapeli wao, lakini wanaotapeliwa kirahisi ni wa kulaumiwa zaidi, hasa ikizingatiwa kuwa wengi wao walishakuwa wahanga wa utapeli kama huo huko nyuma.

Naam, “akili mpya” zinahitajika haraka zaidi pengine kuliko katiba mpya. Naomba nieleweke hapa kwamba simaanishi kuwa watu wengi hawana akili, la hash! Bali neno akili limetumika kumaanisha uelewa.

Isivyokuwa bahati, dunia ya sasa inalazimisha uelewa kuwa siyo suala



Mfano wa Pesa

la hiari, bali la lazima. Mfano rahisi ni katika kupatikana huduma mbalimbali zinazohusisha matumizi ya mtandao wa kompyuta, ambapo mteja hutakiwa kuwa na nywila (password) imara ili kupunguza uwezekano wa akaunti husika kudukuliwa.

Lakini ili kutengeneza nywila imara, ni lazima mhusika ajielimishe japo kidogo kuhusu usalama wa mtandaoni na matumizi ya mtandao kwa ujumla.

Uelewa pia ni muhimu katika kukabiliana na utapeli. Badala ya kuongozwa na tamaa ya utajiri wa haraka, mhusika ataongozwa na kanuni za jinsi ya kupata faida au/na kukwepa hasara, siyo kwa vile ameambiwa na Fulani, bali amethibitisha mwenyewe.

Mwisho, mamlaka husika zichukue hatua kali dhidi ya kampuni zinazojinufaisha kwa kuwatapeli Watanzania.

Walilia fedha zao Ikulu

Na Waandishi WETU

WATANZANIA zaidi wanaelezwa kuwasilisha barua zao Ikulu wakiomba hisani ya Rais Samia Suluhu Hassan kurejeshewa mali na fedha zao wanazodai kuchukuliwa na serikali wakati wa utawala wa Rais John Magufuli.

Wanadai kwamba walichukuliwa mali na fedha zao isivyokuwa halali kwani walilazimika – pengine kwa vitisho, kukubaliana na serikali ili wawe huru kuepuka mateso ya gereza – kwa kupitia utaratibu wa ‘plea bargain.’

Hawa ni baadhi ya watu waliokamatwa, kuswekwa korokoroni na hatimaye kufikishwa mahakamani kwa kufunguliwa mashitaka ya uhujumu uchumi, kutakatisha fedha na au kushirikiana na magenge ya uhalifu.

Pambazuko ambalo limekuwa likifuatilia habari hii kwa muda sasa, limeelezwa na baadhi ya maofisa serikalini kwamba idadi hiyo imekuwa ikiongezeka kwa kuwa wanaoamini kuonewa na kuminywa kwa haki zao, bado wapo wengi.

Gazeti hili limespokeza kwamba baada ya idadi kubwa kubwa, Rais Samia aliamuru kuwepo kwa utaratibu wa kupitia na kuwahoji baadhi ya watu wanaodai kuonewa.

Mtindo wa plea bargain, uliokomazwa na Rais Magufuli wa kukamata na kufikisha mahakamani na hatimaye baadhi kulazimika kuomba msamaha na kulipa fidia, ili kuwa huru, kumeeleza na wanasheria kwamba ulikuwa ni mtindo wa hovy, kuonea na zaidi sana kuvunja sheria.

Mwanasheria Tito Magoti ameeleza kuwa utaratibu wa plea bargain uliofanywa na serikali ya Magufuli ulikuwa unakiuka sheria kwa kuwa msingi wake ni hiyari ya mtuhumiwa na kamwe siyo kulazimishwa wala kuwepo kwa mazingira ya kumfanya afikie hatua



Biswalo Mganga

hiyo ya kuwa huru.

Anasema kutokamilisha upelelezi mapema – baada ya miaka nenda rudi mtu akiwa jela, ni kutengeneza mazingira ya wizi kupitia chaguo pekee la plea bargain ambapo mtuhumiwa hubaki na chaguo hilo tu.

Mwanasheria mwingine, Fatma Karume anaeleza kuwa utaratibu wa plea bargain uliokuwa ukitumiwa na serikali iliyoongozwa na Rais Magufuli (sasa marehemu), ulikuwa ni unyang’anyi kwani ulienda kinyume na taratibu zake.

“Haiwezekani kufanyike plea bargain kwa mtu ambaye serikali inadai uchunguzi wake haujaisha na kwamba anaendelea kushikiliwa na magerezani, haikuwa sawa, hili ni jambo la wazi kabisa kwamba watu walionewa,” anasema Fatma,

Zoezi la kuratibu maombi ya kuangaliwa upya namna “walivyolazimishwa” na kuwepo kwa madai ya kutishwa ili kulipa fidia, linaratibiwa kwa ukaribu zaidi na OFISI ya Rais – Ikulu, Ofisi ya Mkaguzi na Mdhhibiti wa Hesabu za Serikali (CAG) na idara za usalama.

Hata hivyo, Pambazuko limeelezwa kuwa mchakato wa kurejeshewa fedha, kama itathibitika kuwepo uonevu, utachukua muda mrefu kwani kuna kazi kubwa ya kupitia maelezo na vielelezo

Walilia fedha zao Ikulu

Inatoka Uk. 10

vingi kabla ya kufikia uamuzi.

Tayari baadhi ya watu waliokumbwa na kadhia ya kukamatwa, kuteswa na hatimaye kukubali kulipa fedha kwa ajili ya uhuru wao wamethibitisha kuwepo kwa zoezi hilo na kwamba wapo baadhi wanaombwa kuandika maelezo na wengine wakifuatwa na maofisa wa serikali kuchukua maelezo yao.

Mmoja wao ni Erick Kabendera, mwandishi wa habari ambaye alilazimika kulipa Sh. milioni 273 ili kuwa huru baada ya kukamatwa na kushitakiwa kwa makosa ya utakatishaji fedha na ukwepaji kodi huku akiondolewa shitaka la kuongoza genge la uhalifu.

Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, ilimuachia huru Kabendera Jumatatu, Februari 24, 2020, baada ya serikali kukubaliana na “ombi” lake kupitia kwa Mkurugenzi wa Mashtaka Tanzania (DPP) la kulipa fidia ili kuwa huru.

Ilielezwa mahakamani kwamba Kabendera alikiri shitaka la kukwepa kodi ya Sh. milioni 173 na kwamba alikubali kulipa kiasi hicho cha fedha kwa mafungu ndani ya kipindi cha miezi sita. Pia ilielezwa kuwa Kabendera alikiri pia shitaka la utakatishaji fedha na mahakama ilielezwa kuwa mwandishi huyo maarufu alikuwa amelipa mapema Sh. milioni 100 ikiwa faini ya shitaka.

Mwingine aliyekumbwa na kadhia hiyo na kulazimika kuwa huru kwa kuingia makubaliano ya kulipa fedha ni Ofisa wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Tito Magoti na mwenzake Theodory Giyan, Januari 5, 2021. Waliachiwa huru baada ya kukubali kulipa faini ya Sh. milioni 17. Walikamatwa Desemba 2019 na kufunguliwa mashtaka matatu ikiwemo la utakatishaji wa fedha.

Baada ya Kabendera – ambaye sasa anaishi Uingereza, kuombwa kuandika maelezo yake na kufanya hivyo,

ameliambia Pambazuko kwamba ana imani kubwa kwamba haki itatendeka na kila mwenye kustahili haki hiyo huenda akaipata.

“RAIS Samia Suluhu Hassan anaonekana hapendi kuonea mtu. Anapenda haki itendeke na ionekane machoni pa wengi inatendeka kwa uhalali na siyo kuonewa, ngoja tsubiri tuone kitakachoendelea baada ya serikali yake kukamilisha mchakato ambao imeanza,” alisema Kabendera.

Mmoja wa watuhumiwa wa utakatishaji fedha ambaye aliamua kukubali kulipa fidia – na kueleza alilazimishwa, anasema; “Mama (Rais Samia) ni kiongozi ambaye ameletwa kuokoa nchi, tulikosa uhuru, watu walinyang’anya mali kwa ubabe na sasa tunashukuru Rais Samia anakwenda kurekebisha mambo mengi.”

Pamoja na kukataa kutajwa jina gazetini, lakini amepongeza uamuzi huo wa serikali na kwamba ana imani haki ya wanaostahili, itapatikana.

Akizungumzia hatua hii ya serikali kuanza kufuatilia uhalali na haki ya kufanyika kwa plea bargain, Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe amesema; “tunataka haki itendeke. Walioonewa kwa kubambikiwa Kesi na kulipishwa pesa, warejeshewe pesa zao, rekodi yao ya jinai ifutwe na waliohusika na uporaji huu wawajibishwe. Hii itaweka Msingi wa Watu kutoonewa tena.”

Pambazuko linazo taarifa kwamba hadi kufikia Septemba 30, 2020, watu waliokuwa korokoron na walioomba kulipa fidia ili wawe huru hata kabla ya madai yao kukamilika kwa uchunguzi wa kesi zao walikuwa 467.

Katika muda huo - wa hadi Septemba 30, 2020 zaidi ya Sh. bilioni 12 zilikuwa zimekusanywa na ofisi ya DPP, wakati huo ikiwa na mkurugenzi wake, Biswalo Mganga ambaye ilielezwa fedha hizo zilikuwa zikipokelewa na ofisi yake kupitia akaunti maalumu ndai ya Benki Kuu ya Tanzania.

Raila Odinga kurejea bungeni?

**Na Juma NAMLOLA
Taifa Leo**

ALIYEKUWA mgombea urais nchini Kenya kupitia Azimio la Umoja -One Kenya, Raila Odinga na mgombea wakenya wake, Martha Karua huenda wakaingia bungeni.

Wanasiasa hao wanaweza kuingia kwenye vikao vikubwa vya umuzi endapo pendekezo la mwananchi mmoja kutafuta saini milioni moja kupitisha ombi lake litakubaliwa.

Nyongesa Makhanu ameiandikia barua aliyoundikia Tume Huru ya Uchaguzi na Mikapa (IEBC), akiomba ruhusa ya kukusanya sahihi za Wakenya chini ya Kipengee namba 257 cha Katiba.

Kifungu hicho kinaeleza jinsi Katiba inavyoweza kurekebisha kwa kutumia kauli ya wengi. Kwamba marekebisha ya Katiba yanaweza kupendekezwa kupitia ombi linalopaswa kuungwa mkono na saini milioni moja (1,000,000) za Wakenya waliosajiliwa kuwa wapigakura.

Kwa kutumia kifungu hicho, Makhanu anataka idhini ya IEBC ambayo ina uwezo kisheria kutambua wapigakura, ili apendekeze mageuzi ya Katiba, ikiwemo kumteua moja kwa moja anayeibuka mshindi wa pili kwenye uchaguzi wa urais.


Agosti 15, 2022, mwenyekiti wa IEBC, Wafula Chebukati alimtangaza Dkt. William Ruto kuwa mshindi wa urais kwa kupata kura 7,176,141 huku Raila Odinga akiwa wa pili kwa kupata kura 6,942,930.

Hivyo ni wapigakura 233,211 pekee walioamua Dkt. Ruto kuongoza Kenya.

“Kwa kuwa Odinga au mtu yeyote aliyebuka wa pili ana karibu nusu ya wapigakura wote, siyo vyema mtu kama huyo kukosa majukumu kwa kipindi cha miaka mitano,” anaeleza Nyongesa.

Katiba ilivyo sasa hivi, hakuna nafasi ya kiongozi rasmi wa upinzani bungeni.

Inatamka kwamba anayeibuka wa pili,



Raila Odinga

hata kama atakuwa ameshindwa kwa kura moja, huishia kwenye “baridi ya kisiasa” kwa miaka mitano inayofuata, hadi uchaguzi mkuu mwingine ufanywe.

Iwapo IEBC itaidhinisha ombi la Nyongesa ambaye ni mhandisi wa uashi, kisha akusanye saini na kupelekwa bungeni kwa ajili ya kurekebisha sheria kuhusu uwakilishi, huenda Odinga “akafufuka” kisiasa kwa kuteuliwa kuwa mbunge maalum.

Hata hivyo, marekebisha hayo lazima yaundiwe muswada utakaoidhinishwa na IEBC na kupelekwa katika mabunge yote 47 ya kaunti ndani ya miezi mitatu.

Mabunge hayo pia yana miezi mitatu ya kupitisha au kukataa mapendekezo kama hayo. Iwapo yatapitishwa, muswada huo utapelekwa Bunge la Taifa na Seneti na ukipitishwa huko, unakuwa sheria.

Hii ina maana kuwa Odinga atasubiri hadi angalau Aprili 2023 kujua kama atapata nafasi ya kurejea katika jumba aliloliacha mwaka 2012 alipokuwa Waziri Mkuu na mbunge wa Lang’ata.

TanESCO yakoleza umasikini Katavi

**Na Deusdedith KAHANGWA,
Mpanda**

DUARA la ufukara kwa wananchi wa Mkoa wa Katavi huenda likadumu kwa muda mrefu endapo ufumbuzi wa haraka wa upungufu wa nishati ya umeme hautapatikana, Pambazuko limebaini.

Katavi ni mkoa wa mwisho kwa ukusanyaji wa mapato ya kodi kwa mwaka 2020/2021, ikiwa imekusanya Sh. bilioni 5.4 tu kwa mujibu wa takwimu za Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Takwimu zilizopatikana kutoka mkoani humo zinaonyesha kuwa wakati mahitaji ya umeme ni megawati 20, mkoa huu unazalisha megawati tano pekee za umeme, sawa na asilimia 25 za mahitaji ya wateja.

Aidha, Mkoa wa Katavi ‘unahemea’ megawati moja ya umeme kutoka Zambia, kwa ajili ya kuhudumia baadhi ya maeneo ya mkoa.

Uzalishaji wa megawati tano unafanyika kwa kutumia mitambo ya jenereta kadhaa zilizo mkoani humo, mbili zikiwa wilayani Mpanda, na jenereta moja ikiwa nje ya wilaya hii.

Gharama za mafuta ya kuendesha jenereta zilizoko wilayani Mpanda ni Sh. milioni 1.2 kwa mwezi, wakati makusanyo ya mwezi kutokana na mauzo ya umeme unaozalishwa ni Sh. laki nane kwa mwezi. Hivyo, TanESCO mkoani Katavi wanapata hasara ya Sh. 400,000 kila mwezi sawa na hasara ya asilimia 33.

Uchunguzi wa Pambazuko umebaini kuwa, kati ya megawati 21 zinazohitajiwa na wateja mbalimbali, mahitaji ya wawekezaji katika migodi na viwanda ni megawati 16, wakati mahitaji ya wateja wengine kama vile maduka ya biashara na kaya ni megawati tano.

Wawekezaji katika migodi na viwanda wanaohitaji megawati 16, ni pamoja na kampuni ya Katavi Mining, ambayo peke yake inahitaji megawati tisa.

Kwa hiyo, kama wawekezaji katika migodi na viwanda watapatiwa umeme



Wasiri wa Nishati January Makamba.

unaozalishwa kwa sasa, inabidi wateja wengine wote wakatiwe umeme.

Pambazuko limebaini kuwa hivi sasa TanESCO wanasimika jenereta zingine mbili wilayani Mpanda zitakazozalisha megawati 2.5, na hivyo kuuwezesha mkoa kuzalisha jumla ya megawati 7.5, kiata cha umeme ambacho bado hakiwezi kuleta unafuu katika kukidhi mahitaji ya wateja.

Kutokana na kukosekana kwa umeme wa kutosha, wawekezaji wa Katavi Mining Company Limited, wanatumia umeme wa dizeli wanaouzalisha wenyewe huko mgodini.

Pambazuko limeambiwa na uongozi wa mgodi huo kwamba gharama za mafuta ya kuendesha jereta kwa mwezi ni Sh. milioni 800 kwa mwezi, jambo linalosababisha gharama za uendesaji wa mgodi kuwa kubwa zaidi, kuleta faida kidogo, na hivyo kulipa kodi kidogo serikalini.

“Pamoja na jitihada za serikali ya Mkoa wa Katavi kuhamasisha uwekezaji, uhaba wa umeme mkoani humo ni sababu kubwa ya kudhoofisha juhudi hizo,” Ofisa Mipango wa Mkoa wa Katavi, Huruma Mwalutanile, aliliambia Pambazuko.

Kwa mujibu wa Huruma, mkoa huo una fursa tele za uwekezaji zilizobainishwa tangu mwaka 2011 kupitia Mipango wa Mkoa wa Katavi wa Miaka Kumi na Tano Kuanzia 2012 hadi 2026.

TanESCO yakoleza umasikini Katavi

Uwanja wa Ndege wa Mpanda - Picha kutoka Dar24

Mpango huo uliandaliwa enzi za Mkuu wa Mkoa wa Katavi aliyetwa Dkt. Rajab Rutengwe, akiwa anafanya kazi na Katibu Tawala aliyejulikana kuwa ni Mhandisi Emmanuel Kalobelo.

Katika mpango huu, Mkuu wa Mkoa, Dkt. Rutengwe, aliandika tamko lilemalo kwamba, Mkoa wa Katavi “unakabiliwa na changamoto nyingi za kiuchumi na kijamii zinazohitaji msukumo maalum wa kuzitatua.”

Naye Mhandisi Kalobelo, akiwa Katibu Tawala wa wakati huo, akiandika “rai” yake kwenye mpango huo alisema kwamba, “Mkoa wa Katavi ni miongoni mwa mikoa ambayo bado iko nyuma kimaendeleo licha ya kuwa na utajiri wa maliasili”; kwamba, maliasili hizo ni pamoja na “misitu, ardhi, maziwa na madini”; na kwamba, mkoa una “hali ya hewa nzuri kwa kilimo cha mazao ya chakula na biashara pamoja na ufugaji.”

Kwa mujibu wa “rai” ya Kalobelo, “changamoto zinazosababisha mkoa kuwa nyuma kimaendeleo ni pamoja na miundombinu mibovu ya usafirishaji, ukosefu wa nishati ya umeme wa uhakika, upungufu wa watumishi, ukosefu wa soko la uhakika la mazao ya kilimo, uharibifu mkubwa wa mazingira, ukosefu wa viwanda vya kusindika mazao mbalimbali, ukosefu wa wakandarasi wenye sifa na mitaji, na uwekezaji kidogo kwenye sekta za uzalishaji na utoaji huduma.”

Imebainika kuwa tangu 2011 hadi

sasa, sehemu kubwa ya mpango wa miaka 15 haujawahi kufanyiwa mapitio kwa sababu ya ukosefu wa bajeti husika.

Na sehemu nyingine ya majibu hayo ni “Mwongozo wa Uwekezaji Katika Mkoa wa Katavi,” wa mwaka 2019, uliosainiwa na Mkuu wa Mkoa wa wakati huo, Juma Zuberi Homera.

Mwongozo huu unawaalika wawekezaji kwa ajili ya kuwekeza kwenye maeneo yafuatayo; kujenga viwanda kwa ajili ya kuchakata na kusindika mbegu za mafuta, nafaka, matunda, ngozi, nyama, asali, samaki, na fenicha.

Hata hivyo, mwongozo huu unabainisha uwepo wa changamoto ya umeme pale unapotamka kwamba, Mkoa wa Katavi umeunganishwa “kwenye mfumo wa umeme unaozalishwa kwa kutumia jenereta za mafuta ya dizeli.”

Pambazuko lilimwomba Meneja wa TanESCO wa Mkoa wa Katavi, Seraphine Lyimo, aeleze kwa nini tangu 2019 hadi 2022 bado serikali haijaweza kuunganisha Katavi “kwenye mtandao wa gridi ya umeme wa Taifa,” kama mwongozo wa uwekezaji ulivyobainisha.

Meneja huyo amesema kuwa mpango wa kuunganisha Mkoa wa Katavi kwenye gridi ya umeme wa Taifa unaendelea kutekelezwa, tangu 2020 ulipozinduliwa na aliyekuwa Rais John Magufuli.

Hapa, Lyimo alitaja mradi wa kujenga njia kuu ya kusafirisha umeme kutoka Tabora hadi Katavi, wenye umbali wa kilometa 381.

TanESCO yakoleza umasikini Katavi

Inatoka Uk. 14

“Mradi huu utasafirisha msongo wa umeme wenye ukubwa wa 132KVA, ambapo, baada ya umeme kupoozwa, Mkoa wa Katavi utapokea msongo wa umeme wenye ukubwa wa 33KVA,” anabainisha.

Kwa mujibu wa Lyimo, Mradi wa Tabora-Katavi ambao unatekelezwa na kampuni tanzu ya TanESCO iitwayo ETDCO, unasimamiwa na kitengo cha uwekezaji kilichoko makao makuu ya TanESCO, Dar es Salaam. Mradi huu utakamilika Desemba 2023, yaani miezi 14 ijayo.

Alipoulizwa endapo, kati ya sasa na Desemba 2023, TanESCO ina mpango wa muda mfupi wa kuwapatia umeme wawekezaji, Lyimo alisema; “kwa sasa tunaweka jenereta mbili kwenye kituo chetu cha Mpanda. Zikikamilika zitaongeza megawati 2.5 kwenye mfumo wa umeme.

... Hivyo tutakuwa na uzalishaji wa megawati 7.5. Megawati tano tayari ni kwa ajili ya wateja wa kawaida. Na mteja anayetaka megawati 9 huwezi kumpa pungufu. Kwa hiyo, wawekezaji wanaotaka umeme mwingi watapaswa kuendelea kusubiri hadi mradi wa Tabora-Katavi utakapokamilika Desemba 2023.”

Alipoulizwa endapo inawezekana kuharakisha utekezaji wa mradi huo

kwa kuongeza watendaji na kupanua bajeti, Lyimo alisema mwenye majibu kwa swali hilo ni meneja wa mradi aliyeko Dar es Salaam.

Kama serikali haitafanya juhudi za kupitia upya ratiba ya utekezaji wa mradi wa Tabora-Katavi, Mkoa wa Katavi utandelea kusumbuliwa na uhaba wa umeme, kwa kiasi cha upungufu wa asilimia 75 ya mahitaji halisi, kwa miezi 14 ijayo.

Upungufu huu maana yake ni kwamba, duara la ufukara litazidi kuimarika mkoani humo; uzalishaji duni, kodi duni, huduma duni za kijamii, rasilimali watu duni, na hatimaye uzalishaji duni na sababu kuu ikiwa ni umasikini wa umeme

Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Mpanda, Sophia Kumburi, ameliambia gazeti la Pambazuko kwamba; “sisi tunayo mipango mizuri, tuko tayari kwa kazi, isipokuwa kama tutakwamishwa na vikwazo vilivyvo nje ya uwezo wetu.”

Akiongea na Pambazuko, mkazi mmoja wa Mpanda, Julius Imele, ameliambia Pambazuko kwamba; “kama uhaba wa nishati ya umeme ulioko hapa pia upo kwenye mikoa mingine, basi, ujio wa Tanzania ya viwanda utachukua miaka mingi, na tuache kuwa tunaongelea Mapinduzi ya Nne ya Viwanda, wakati bado tunatumia dizeli kuendesha mitambo ya uzalishaji.”



Mitambo ya kupoza umeme

Ng'ambo ni asali ama shubiri?**Na Godwin CHILEWA**

MIAKA kumi na tano iliyopita neno "wabeba boksi" lilikuwa halibanduki mdomoni mwa vijana wa Dar es Salaam na vitongoji vyake.

Neno hili lilitajwa kila kijana wa Kitanzania anayeishi Marekani, au nchi za Ulaya aliporudi nyumbani kusalimbia, na hatimaye kuonekana katika kumbi za starehe. Lilikuwa jina la kejeli na dharau lililoshusha thamani ya wanadiaspora.

Kwa kifupi jina 'wabeba boksi' lilitokana na ukweli kwamba wakati huo idadi kubwa ya vijana walioenda Marekani na Ulaya kuanzia mwanzoni mwa mwaka 2000, walikuwa hawajafanikiwa kupata ajira rasmi (za kitaalam).

Wengi walifanya kazi za vibarua katika viwanda, maduka makubwa, hoteli na sehemu nyinginezo zinazohitaji ajira za muda mfupi bila masharti magumu. Kwa ujumla vijana waliokuwa ughaibuni wakati huo walikula kwa jasho hasa!

Pengine ajira hizo zisingekuwa kigezo cha dharau na kejeli kama hali ya maisha ya vijana wa nyumbani wakati huo ingekuwa ngumu, kama ilivyo sasa.

Lakini wakati huo maisha yalikuwa nafuu sana. Vijana wengi waliokuwa Tanzania walikuwa na pesa kutokana na "mishemishe" walizokuwa wakizifanya.

Kama utakumbuka vyema wakati huo ndipo Tanzania ilipokuwa kinara wa biashara haramu ya dawa za kulevyia, ujambazi, utapeli na biashara nyingi za ujanjaujanja.

Kipindi hicho pia ndipo pesa za kashfa za Richmond na nyinginezo zilipokuwa zikizunguka mitaani. Vijana wajanja wa mjini walitengeneza pesa kwa kila namna; kwa njia halali na haramu.

Ni wakati huo, pesa ilizunguka kutoka kwa mafisadi hadi kwa mama ntilie. Maisha ya watu wengi wa kawaida yalikuwa rahisi kwani 'chungu' kilikuwa wazi.

Siyo ajabu vijana waliokuwa wakitafuta pesa kwa jasho huko

*Mfanyakazi*

ughaubuni walidhihakiwa kwa kuitwa wabeba boksi, na hakuna kijana wa mjini aliyetamani kwenda Marekani au Ulaya. Akafanye nini?

Lakini mambo sasa yamebadilika, leo hii miaka kumi na tano baadae, vijana waishio ughaibuni (wanadiaspora) waliokuwa wakiitwa wabeba boksi, sasa wanaitwa "wawekezaji" na wale "washua - mapedezhee" wa mjini waliokuwa wakitamba miaka ile, wengi wao wamefifia au kufilisika kabisa.

Hali ya vijana wengi wa nyumbani imekuwa ngumu kiasi cha kuanza kuwaheshimu wanadiaspora, na wengine kufanya jitihada za kukimbilia ughaibuni, ambako miaka michache iliyopita walikuwa hawataki hata kupasikia.

Je, ni nini kilichowasibu? Jambo gani la ajabu lililotokea hapo katikati? Au ni mabadiliko gani yaliyosababisha hili? Hapo ndipo mara nyingi huwa nawaambia wanaoniuliza maswali watafute majibu wenyewe.

Wajiulize kama kweli Marekani ni nchi ya maziwa na asali, yaani nchi ya fursa au mahali pa utumwa wa karne mpya?

Mwandishi wa safu hii ni Mtanzania anayeishi na kufanya shughuli zake Texas, Marekani.

Tutakumbuka daima...



Mjukuu wa Abeid Amani Karume, Rais wa Kwanza wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na mtoto wa Rais (awamu ya sita) Amani Abeid Karume, Wakili Fatma Karume, akiwa na Mwalimu Julius Nyerere alipokwenda kumsabahi nyumbani kwake Msasani, Dar es Salaam. Picha hii ilipigwa mwaka 1986. (Picha kutoka maktaba ya Fatma).

‘Dkt. Biteko asivimbe kichwa’**Na Shabaan LULELA**

SIFA za kutenda kazi kwa bidii, uwazi, ubunifu na kuegemea teknolojia, ni miongoni mwa mambo ambayo yanaendelea kumpa Waziri wa Madini, Dkt. Doto Biteko nguvu ya kupongezwa.

Amekuwa akipongezwa; siyo tu wadau wa sekta ya madini, taasisi anazoshirikiana nazo, bali hata wananchi wengi wanaoifuatilia utendaji kazi wa wasaidizi wa rais.

Katika kuimarisha sifa za Biteko, jana Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa eneo la Runzewe, Bukombe mkoani Geita, alimwaga sifa kedekele kwa Dkt. Biteko kwa kumuelezea kwamba ni “kijana mchapa kazi.”

Rais Samia akawaeleza Watanzania kwamba siri ya kutomhamisha wizara au kumuondoa Dkt. Biteko ni kuridhishwa na utendaji wake.

“Ndiyo maana mnaona nawagusa wote (mawaziri) nawabadilisha, lakini Biteko yupo hapo Wizara ya Madini kwa sababu ni kijana anayefanya kazi nzuri,” aliongeza Rais Samia.

Kupewa sifa kwa Dkt. Biteko, kunatokana na rekodi aliyoiweka kwenye wizara hiyo baada ya kuwepo kwa mabresho ambayo yameweza kuongeza mapato ya serikali kutokana na madini.

Katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2021 wastani wa mchango wa sekta hii umekua hadi kufikia asilimia 7.3 ya Pato la Taifa, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2020.

Aidha, katika robo ya tatu (Julai – Septemba) mwaka 2021, mchango wa sekta ya madini uliongezeka hadi kufikia asilimia 7.9 ya Pato la Taifa kutoka asilimia 7.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2020.

Mbali na hivyo, ndani ya kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa serikali ya awamu ya sita, sekta ya madini imeweka historia kwa kushuhudia mauzo ya moja kwa moja yenye thamani ya Sh. trilioni



Waziri wa Madini, Dkt. Doto Biteko

8.3 kutokana na mauzo ya madini ya aina mbalimbali.

Mauzo hayo yanatokana na madini ya dhahabu, fedha, shaba, makaa ya mawe, madini ya vito na madini ya ujenzi na viwandani.

Pia katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, wizara hiyo imekusanya Sh. bilioni 597.53 ikiwa ni maduhuli ya serikali.

Pamoja na sifa hizo kwa Dkt. Biteko, lazima atambue kuwa bado ana kazi kubwa mbele yake. Asiwe kama mgema, kwamba anaposifiwa, basi tembo huja kulitia maji.

Ni katika sifa hizo, Dkt. Biteko anapaswa kuongeza bidii zaidi, kushirikisha wasaidizi wake na wadau ili kukuza mapato ya madini na kamwe asiwe na kiburi kilicholewa sifa kutoka kwa Rais Samia na hata wadau wa madini.

Ni kipindi hiki anapaswa kudhihirisha kwa dunia kuwa sifa anazopewa siyo za bahati mbaya wala “nguvu ya soda,” bali ni kujitoa kutumikia Tanzania na watu wake.

Dkt. Biteko kamwe “asivimbe kichwa” katika kuonyesha utumishi uliotukuka, lazima aongeze juhudi na ubunifu kudhibiti utoroshwaji wa madini, kukomesha rushwa na kuongeza namna bora na salama kwa wachimbaji wadogo kupata mikopo yenye riba nafuu kutoka benki.



Ukanushi katika Njeo Ijayo

Na Dkt. Michael MASHAURI

KISWAHILI ni miongoni mwa lugha zinazokua kwa kasi kubwa kila siku duniani. Vyuo vikuu nje ya Afrika, vimeanza kufunza lugha hiyo adhimu. Kutokana na umuhimu wake, Pambazuko limeamua – kila wiki, kuwa njia ya kufundisha Kiswahili bure kwa yeyote anayependa.

Leo tunajifunza kuhusu kiambishi cha ukanushi katika njeo ijayo (Negation in Future Tense) ni Ha- kinachofuatiwa na kiambishi cha nafsi na kiambishi cha njeo

ijayo ta- isipokuwa nafsi ya kwanza umoja inayotumia si- na hudondosha kiambishi cha nafsi.

Nafsi ya pili umoja inaweza kutumia hau- au hu- na nafsi ya tatu umoja hudondosha kiambishi cha nafsi -a. (Prefix for negation in future tense is Ha- which is followed by the personal and future tense prefixes except for first person singular which uses si- and drops the personal prefix. The second person singular can use hau- or hu- and the third person singular drops the personal prefix a-.)

Examples			
1 st Person	Singular	Affirmative	Nitaimba wimbo (I will sing a song)
		Negative	Si aimba wimbo (I will not sing a song)
	Plural	Affirmative	Tutakimbia ufukweni (We will run on the beach)
		Negative	Hatut akimbia ufukweni (We will not run on the beach)
2 nd Person	Singular	Affirmative	Wewe utapika chapati (You will cook chapati)
		Negative	Wewe hut apika chapati (You will not cook chapati) Wewe haut apika chapati (You will not cook chapati)
	Plural	Affirmative	Nyinyi mtacheza muziki (You will dance music)
		Negative	Nyinyi ham tacheza (You will not dance music)
3 rd Person	Singular	Affirmative	Yeye atienda Dar es Salaam (He/she will go to Dar es Salaam)
		Negative	Yeye hata ienda Dar es Salaam (He/she will not go to Dar es Salaam)
	Plural	Affirmative	Wao watasoma kitabu (They will read a book)
		Negative	Wao haw atasoma kitabu (They won't read a book)

Kwa nomino za ngeli nyingine, ukanushi hujitokeza kama inavyooneshwa katika jedwali hapa chini. (For nouns from other noun classes, negation appears as in the table below.)

Examples			
Singular	Affirmative	Mti utakua (A tree will grow)	
	Negative	Mti haut akua (A tree will not grow)	
Plural	Affirmative	Miti itakua (trees will grow)	
	Negative	Miti hait akua (trees will not grow)	

• **Mwandishi wa Darasa la Kiswahili ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.**

Kumbukuzi ya Nyerere



Oktoba 14, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan aliungana na Watanzania kumkumbuka muasisi wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyefariki miaka 23 iliyopita.

JUU: Samia, makamu wake, Dkt. Philip Isdor Mpango, baadhi ya viongozi wa kitaifa na waumini wa Kanisa Katoliki katika Kanisa Kuu la Bukoba, waliungana kuadhimisha kumbukizi ya Mwalimu Nyerere mjini Bukoba, mkoani Kagera. (Picha zote na Iku).

Tendo la ndoa na umoja wa mwili

SERA ya Afya ya Tanzania (2017) haitambui kingamimba kama zana mojawapo ya kupanga uzazi

Sera hii ilitengenezwa wakati wa utawala wa Rais John Magufuli aliyekuwa muumini wa fundisho kwamba - “mke na mume ni mwili mmoja usiopaswa kutenganishwa kwa kutumia kingamimba.”

Katika makala haya najenga hoja ya kifalsafa kukosoa fundisho kwamba jazi wa mume na mke ni mwili mmoja wa kibayolojia.

Nitafanya hivyo kwa mujibu wa mawazo ya mwanafalsafa Aristotle wa Ugiriki ya Kale, aliyeshi kabla ya kuzaliwa kwa Kristo.

Hasa, nitatumia majibu yake kuhusu “kitendawili cha umoja wa tabaka na utofauti wa mnyumbuliko wake.”

Tuanzie katika swali hili: kuna ufanano gani na utofauti upi kati ya mbuzi, saa ya ukutani inayotumia kamani, na timu ya mpira wa miguu?

Kuhusu ufanano, kila kimoja ni kitu chenye sehemu kadhaa zinazofanya kazi tofauti, lakini kwa kushirikiana bila kushindani, kwa ajili ya kutimiza lengo la pamoja.

Sifa hii ndio inaviweka vitu hivyo vitatu katika tabaka kuu moja la vitu nitakaloliita “tabaka la oganizimalia,” yaani “the class of organisms.”

Ndani ya hili tabaka kuu kuna matabaka madogo kama vile tabaka dogo la oganizimalia wa kibayolojia, tabaka dogo la oganizimalia wa kimakanika, tabaka dogo la oganizimalia wa kijamii, na tabaka dogo la oganizimalia wa kiroho.

Katika tabaka dogo la oganizimalia wa kibayolojia kuna watu, mbuzi, kuku, mimea, na kadhalika.

Kwenye tabaka dogo la oganizimalia wa kimakanika kuna saa ya ukutani, gari, ndege ulaya, treni, pikipiki, na kadhalika.

Katika tabaka dogo la oganizimalia ya kijamii kuna timu ya mpira, familia, kampuni, azaki, taifa, na kadhalika.

Na kwenye tabaka dogo la oganizimalia



Aristotle

wa kiroho kuna utatu mtakatifu, jeshi la malaika, ushirika wa watakatifu, na kadhalika.

Kwa mujibu wa Aristotle, umoja wa matabaka haya madogo unatokana na ufanano uliomo kwenye mnyumbuliko wake.

Kwa mfano, viungo vya mwili wa mbuzi ni “ogani” (organs) zinazotimiza lengo la kustawisha uhai wa mwili wa mbuzi.

Hivyo, mbuzi ni mnyumbuliko kwenye tabaka dogo la oganizimalia wa kibayolojia (biological organisms), lenye miili ya kibayolojia (biological bodies), kila mwili ukiwa na umoja unaotokana na lengo maalum, mfano, lengo la kustawisha uhai wa mbuzi.

Kwa mfano tena, vijenzi vya saa ya ukutani ni “ogani” zinazotimiza lengo la kuhesabu majira.

Hivyo, saa ni mnyumbuliko ulioko kwenye tabaka dogo la oganizimalia wa kimakanika (mechanical organisms), lenye miili ya kimakanika (mechanical bodies), kila mwili ukiwa na umoja unaotokana na lengo maalum, mfano, lengo la kuhesabu majira kwa kutumia saa.

Na kwa mfano tena, wachezaji wa timu ya mpira ni “ogani” zinazotimiza lengo la

Tendo la ndoa na umoja wa mwili*Inatoka Uk. 21*

ushindi wa timu.

Hivyo, timu ya mpira ni mnyumbuliko kwenye tabaka dogo la oganizimalia wa kijamii (social organisms), lenye miili ya kijamii (social bodies), kila mwili ukiwa na umoja unaotokana na lengo maalum, mfano, lengo la kutafuta ushindi wa timu ya mpira.

Hivyo, katika mifano mitatu hapo juu, chimbuko la umoja wa kimwili, bila kujali kama tunaongelea mwili wa kimakanika, mwili wa kibayolojia au mwili wa kijamii, unatokana na uwepo wa lengo moja linalotimia kutokana na ushirikiano wa vijenzi vya kitu husika.

Hata hivyo, japo lengo la pamoja ni sifa ya lazima katika kutambulisha umoja wa kimwili (biological individuality), lakini bado haitoshelezi kutambulisha kikamilifu umoja huo, kama nitakavyoonyesha.

Na kwa ajili hii nitatumia mfano wa umoja wa mwili wa mbuzi kudadisi mantiki ya umoja wa mwili wa kibayolojia, na hatimaye kutumia hitimisho husika kuchunguza kama jozi ya mume na mke inatimiza vigezo hivyo.

Hatimaye nitaonyesha kuwa vigezo hivyo havitimii.

Kulingana na fundisho la Aristotle kuhusu umoja wa kimwili, mwili wa oganizimalia kama vile mbuzi unayo sifa ya umoja wa kibayolojia kwa sababu zifuatazo:

Mosi, mwili wa mbuzi ni mnyumbuliko ndani ya tabaka la wanyama wengine wa jamii yake, yaani, ni mnyumbuliko ndani ya tabaka la mbuzi.

Pili, mwili wa mbuzi unayo mipaka ya kijiografia (spatially localised) kwani unashika kipande cha nafasi kilicho mahali fulani na chenye ujazo maalum.

Tatu, mwili wa mbuzi unayo mipaka ya kimajira (temporally localised) kwani unashika kipande cha muda kuanzia tarehe moja ya kuzaliwa hadi tarehe nyingine ya kufa na yenye kumaanisha umri maalum.

Ne, mwili wa mbuzi unaziba nafasi



Ndoa

yote uliyoikalia na hivyo kuzuia vitu baki kukalia nafasi hiyo (spatially continuous).

Tano, mwili wa mbuzi unao umri endelevu, kiasi kwamba, kati ya tarehe ya kuzaliwa na tarehe ya kufa, hakuna pengo la maisha kutokana na kufa na kufufuka kwake, kama ambavyo mito hukauka wakati wa kiangazi na kufufuka wakati wa masika (temporally continuous).

Sita, mwili wa mbuzi unavyo viungo anuwai vyenye kusukumana kwa mujibu wa kanuni ya sababu na matokeo (heterogeneous causally related parts). Mfano, mapafu yachota hewa na kuupa moyo na moyo unasambaza mwilini.

Saba, mwili wa mbuzi unao mfumo mmoja wa neva (single nervous system).

Nane, katika mwili wa mbuzi ukikata ngozi ya paja na kupachika tumboni mwake (grafting) inashikamana. Lakini, ngozi ya mbuzi baki haitagandamana.

Tisa, mwili wa mbuzi una mfumo wa vinasaba vya aina moja (genetically homogeneous)

Na kumi, mwili wa mbuzi ulizaliwa kutokana na tendo la ngono kati ya wazazi wake, naye mbuzi atazaa watoto wanaomfanana kwa njia hiyo.

Hizi ndizo sifa kumi za tabaka la vitu vyenye mwili mmoja wa kibayojia.

Katika tabaka hili kuna mnyumbuliko kama vile James, Jane, sungura, dagaa, tembo, baba James, na mama James.

Kila mnyumbuliko unazo sifa kumi zilizotajwa hapo juu.

Verckys aaga dunia

Na Aboubakary LIONGO

DUNIA inayovutiwa na muziki wa rhumba na kuwa na mapenzi na sauti za saksafoni, hasa kutoka Afrika ya Kati, iko katika maombolezo makubwa.

Kilio cha wapenzi hao wa muziki kinatokana na kifo cha Verckys Kiamuangana Mateta, mwanamuziki mkubwa kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Mateta, jina kubwa katika Afrika, Ulaya na Karibeani -almaarufu kwa kupuliza saksafoni, amefariki Ijumaa iliyopita, wakati akiendelea na matibabu jijini Kinshasa, baada ya kupatwa kiharusi miezi minne iliyopita.

Verckys (78) amefariki akiwa ameacha sifa ya kupigiwa mfano kwa kuwa alitendea haki taaluma yake ya muziki kiasi cha kuwekwa katika “kapu la uchawi wa saksafoni” akiwa pamoja na Manu Dibango.

Pamoja na kuutendea haki muziki, Mateta pia alikuwa mfanyabiashara mkubwa DRC akijihusisha na kuuza vifaa vya muziki, nguo na samani katika miji mikubwa ya nchi hiyo iliyoko Afrika ya Kati.

Alimiliki band kadhaa zilizotamba katika miaka ya 70 na 80 kama vile, Orchestra Veve, Lipua-Lipua na Kiam.

Pia alimiliki studio ya kurekodi iliyokuwa ikiitwa Edition Veve ambayo bendi nyingi maarufu enzi hizo zikiwemo Lipua-Lipua, Les Kamale, Shama Shama, Bella Bella, Kiam, Zaiko Langa Langa zilirekodi nyimbo zao kwake.

Amewacha familia kubwa ya watoto 32, wengi wakiwa wanaishi Ufaransa, Brazil na Canada, baadhi wako Afrika. Miongoni mwa watoto wake, ni wawili; Ancy na Daniel ndiyo wanajihusisha na kazi ya baba yao.

Ancy ambaye anaishi Uingereza, ameurekodi upya wimbo wa baba yake ‘Nakomituka,’ ambao ulimletea



Verckys Kiamuangana Mateta,

matatizo Verckys na Kanisa Katoliki nchini DRC baada ya mashairi kudaiwa na kanisa hilo kuwa na chembe ya “dhihaka.”

Sehemu ya mashairi hayo inahoji, iweje picha nyingi zinazotumiwa na kanisa hilo kuonyesha shetani ni mweusi, huku malaika wote wakitambulishwa kuwa wazungu?

Mwaka jana, Verckys akiwa na miaka 77, alingia kwenye mgogoro na watoto wake baada ya kuoa binti wa miaka 25, ingawa aliwashinda na kuendelea kuishi na mkewe huyo mwenye umri mdogo.

Alale salama Verckys huku dunia ikiendelea kumuenzi kupitia muziki wake.

Mwandishi wa makala haya ni mjumbe wa Jukwaa la Wahariri na mmoja wa viongozi wa Moonlight Media. Imehaririwa kukidhi viwango na nafasi ya Pambazuko.

PICHA KUBWA



KULEA MWANA: Tembo wakimlea mtoto katika mbuga ya Etosha iliyoko Namibia. Picha hii imepigwa na Claudia Lothering na kuchotwa kutoka DailyMarverick.

Mhariri wa Pambazuko, anaomba wasomaji wenye mapenzi na kupiga picha watume kwake ili zitumike (Tuma kwa email; info@pambazuko.tz). Mtuma picha anatakiwa kuwa ndiye mpigaji na aweke maelezo.

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi na Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

